



## TAARIFA KWA UMMA

### USAJILI WA WAFANYABIASHARA WA BIDHAA ZA TANZANIA WENYE ULEMAVU KUSHIRIKI KWENYE DUKA MAALUM "BAZAAR" KATIKA MAONESHU YA DUNIA (EXPO 2020 DUBAI)

Dar es Salaam, 24 Machi, 2020

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) inapenda kuwataarifu wafanyabiashara wa bidhaa za kitanzania **WENYE ULEMAVU** kuwa Waandaaji wa Maonesho ya Dunia ya mwaka 2020 kutoka Nchi ya Falme za Kiarabu (EXPO 2020 Dubai) wameipa Tanzania Eneo la kuuzia Bidhaa zake (Bazaar).

TanTrade inawakaribisha **WENYE ULEMAVU** ambao ni Wazalishaji wa bidhaa za Kahawa, Bidhaa za Ngozi, Chai, Viungo (Spices), Matunda na Mboga zilizokaushwa, Nafaka (Maharage, mchele, unga wa muhogo uliyofungashwa kwenye ujazo wa gramu 500 au kilo moja tu), Mwani (Uliokaushwa au wa Unga), Asali, Korosho, Mafuta ya Nazi, Madini, vikapu, vipepeo, mikeka, makawa, shanga (herini, mikufu, bangili), khanga, vipodozi, usindikaji wa vyakula (pilipili za embe, ukwaju, ndimu, mbilimbi n.k) kutuma maombi yao sasa.

Washiriki **WENYE ULEMAVU** wa Bazaar wanatakiwa wawe na vigezo vifuatavyo ambavyo vimewekwa na Waandaaji Mamlaka ya Expo 2020 Dubai:

#### **A. Masharti ya Bidhaa**

- i) Wazalishaji wa bidhaa zinazotokana na malighafi hai (organic), watatakiwa kuwasilisha nakala ya cheti cha mali hai *organic* kutoka Taasisi inayosimamia na ripoti ya maabara kuthibitisha ubora wa bidhaa hizo;
- ii) Bidhaa zote zenye uwezo wa kuliwaza au kutibu mfano (herbal tea, herbal coffee) zitalazimika kukaguliwa na Waandaji na Mzalishaji atalazimika kutoa maelezo ya kina kuhusu utengenezaji wake na malighafi zote zilizotumika (chemical + genetically composition)
- iii) Bidhaa zote lazima ziambatane na maelezo ya malighafi yote na kemikali zilizotumika
- iv) Bidhaa zote za vyakula na vinywaji lazima ziambatishwe na vyeti vya afya (health certificate) kutoka Mamlaka husika
- v) Bidhaa zote lazima ziwe zimethibitishwa na TBS na ZBS

- vi) Bidhaa zote za vipodozi lazima ziwe zimethibitishwa na TBS, ZFDA
- vii) Bidhaa zote zinazotokana na wanyama na ndege lazima ziambatishwe na yafuatayo:-
- Cheti cha Asili iliyotolewa na Mamlaka yenye uwezo katika nchi ya asili
  - Cheti cha Afya na Mamlaka inayofaa katika nchi ya Asili
  - Hati ya Matibabu (Mafuta, Kemikali au Chumvi) iliyotolewa na Mamlaka inayofaa kutoka nchi ya Asili ili kuthibitisha kuwa bidhaa hiyo imetibiwa
  - Cheti cha Halal
  - Ikiwa bidhaa imetokana na mnyama aliyetajwa kwenye orodha ya Mkataba wa Kimataifa wa Spishi zilizo hatarini (CITES) cheti au ripoti kutoka Nchi Asili lazima iambatishwe

**B. Masharti ya Lebo:-**

- i) Bidhaa zote zinatakiwa kuwa na lebo zenye maelezo ya kina ya bidhaa (chemical and genetically composition) ikiwemo jina la bidhaa, nembo, rajamu, uzito, wingi, nchi zilikotoka, malighafi zilizotumika, tarehe za kuzalishwa na kuharibika (electronic production and expiry date) lebo zote ziwe zimechapishwa kitaalamu ikijumuishwa na *nutrition content* (madini, mafuta, wanga, protini n.k)
- ii) Bidhaa zote ziwe na alama ya msimbo milia (Barcode) kutoka GS1

**C. Masharti ya Vifungashio:-**

- i) Vifungashio vyote vya bidhaa viwe vyenye ubora wa kimataifa ambavyo vitailinda bidhaa kutokana na mshituko, kupasuka, kuvuja, upotevu wa ubora na kuweza kuhimili mabadiliko ya hali ya hewa
- ii) Vifungashio vyote vya bidhaa viwe na uwezo wa kuhimili mikiki ya usafirishaji wa majini, angani na barabarani
- iii) Vifungashio vya usafirishaji ni lazima vikaguliwe ili kuhakikisha vina ubora wa kimataifa na havitapitisha unyevunyevu, kutengeza fangas, kupenyeza wadudu n.k.
- iv) Washiriki wanahimizwa kutumia vifungashio vyenye ubora wa hali ya juu na vinavyozalishwa na malighafi ambayo inaweza kutumika mara dufu (recycled)

Endapo bidhaa yako inakidhi vigezo tajwa hapo juu, tafadhali pakua fomu kupitia [www.tantrade.go.tz](http://www.tantrade.go.tz) na uwasilishe katika Ofisi za Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) kabla ya tarehe 18 Aprili 2020 ukiambatisha sampuli ya bidhaa yako, lebo na nakala ya vibali vyote kutoka Mamlaka husika. NB: Bidhaa tajwa tu ndizo zitakazoruhusiwa.